

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA TATU

YATOKANAYO NA KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI

30 MEI, 2016

MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI

TAREHE 30 MEI, 2016

I. DUA:

Saa 3.00 Asubuhi Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) alisoma Dua na Kuongoza Bunge.

Makatibu Mezani:

1. Dkt. Thomas Kashilillah
2. Ndg. John N. Joel
3. Ndg. Neema M. Wankanga
4. Ndg. Charles Mloka
5. Ndg. Joshua Chamwela

II. KIAPO CHA UAMINIFU:

Wabunge wafuatao waliapishwa:-

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
3. Mhe. Machano Othman Said
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir

III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

1. Mhe. Susan Alphonse Kolimba aliwasilisha Mezani Taarifa ya Mwaka ya Hesabu za Kituo cha Kimatifa cha Mikutnao cha Arusha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.
2. Mhe. Susan Alphonse Kolimba aliwasilisha Mezani Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki Kikanda na Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
3. Mhe. George Huruma Mkuchika, aliwasilisha Mezani taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu baadhi ya Wabunge kufanya vurugu Bungeni na kudharau Mamlaka Spika ya tarehe 27 Januari, 2016.

IV. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa:-

OFISI YA WAZIRI MKUU:

Swali Na.257 – Mhe. Fatma Hassan Toufiq

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Fatma Hassan Toufiq
(ii) Mhe. Edwin Mgante Sannda

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na.258 – Mhe. Felister Aloyce Bura

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Felister Aloyce Bura
(ii) Mhe. Esther Nicholas Matiko
(iii) Mhe. Josephine Johnson Genzabuke

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

Swali Na.259 – Mhe. Josephine Genzabuke [kny. Mhe. Augustino Vuma Holle]

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Josephine Genzabuke
(ii) Mhe. Musukuma Joseph Kasheku
(iii) Mhe. Samson Kasuku Bilago
(iv) Mhe. Alex Raphael Gashaza

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

Swali Na.260 – Mhe. Leonidas Tutubert Gama

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Leonidas Tutubert Gama
(ii) Mhe. Leah Jeremiah Komanya
(iii) Mhe. Susan Anselm Lyimo

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

Swali Na.261 – Mhe. Khatib Said Haji

Swali la nyongeza: Mhe. (i) Mhe. Khatib Said Haji
(ii) Mhe. Joseph Roman Selasini

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Swali Na.262 – Mhe. Stella Ikupa Alex

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Stella Ikupa Alex
(ii) Mhe. Boniphace Mwita Getere

Swali Na.263 – Mhe. Hassan Elias Masala

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Hassan Elias Masala
(ii) Mhe. Joseph Leonard Haule
(iii) Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:

Swali Na.264 – Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza

Swali la yongeza: (i) Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Swali Na.265 – Mhe. Peter Joseph Serukamba

Swali la yongeza: Mhe. Peter Joseph Serukamba

MATANGAZO:

- Wageni wote waliokuwepo Bungeni walitambulishwa.
- Kamati ya LAAC itakuwa na Kikao saa 7.00 mchana Ukumbi wa Msekwa D
- Wabunge wanaotoka Kambi ya Upinzani wakutane saa 7.00 mchana Msekwa
- Matokeo ya Mechi kati ya Bunge na NMB yalitangazwa.

V. TAARIFA (KAULI YA SERIKALI):

- Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi alitoa Taarifa kuhusu suala la kurudishwa nyumbani kwa Wanafunzi wa UDOM kutokana na mgomo wa Walimu.

MWONGOZO WA SPIKA:

Wabunge wafuatao waliomba mwongozo wa Spika:-

- 1) Mhe. Juma Selemani Nkamia alitumia Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo kuhusu suala la kurudishwa nyumbani kwa wanafunzi wa UDOM kwa kosa ambalo siyo lao na kuhoji kwa nini Serikali isingetatua tatizo la walimu ambao ni wachache na badala yake ikaamua wanafunzi waondolewe tena kwa masaa 24.

Naibu Spika alieleza kuwa Serikali imeshatoa taarifa wanalijua suala hilo na wanalifuatilia.

- 2) Mhe. Joshua Samuel Nassari aliomba mwongozo kupitia Kanuni ya 68(7) 6(9)(1) na 47(1) kuhusiana na suala la wanafunzi wa UDOM, pia alitoa hoja kwamba Bunge liahirishe mjadala ili kujadili jambo la dharura kuhusiana na kuondolewa Chuoni kwa wanafunzi hao.

Naibu Spika alitoa mwongozo kuwa suala hilo siyo la dharura. Wakati bado anaendelea kutoa maelezo yake kuhusu mwongozo huo, baadhi ya Wabunge wa Upinzani na Wabunge wa Chama Tawala walianza kuzomea na kupiga kelele, hata baada ya kuamliwa watoke nje waliendelea kuzomea.

VI. KUSITISHA BUNGE:

Kutokana na vurugu hizo, Naibu Spika alisitisha Bunge hadi Saa 10.00 jioni.

VII. BUNGE KUREJEA:

- Saa 10.00 Bunge lilirejea na kuongozwa na Naibu Spika, Mhe. Dkt. Tulia Ackson.
- Naibu Spika alianza kwa kutoa maelezo ya maamuzi ya kikao cha Kamati ya Uongozi kilichokaa kuzingatia suala la mwongozo juu ya wanafunzi wa UDOM, ambapo alieleza kuwa Kamati ya Uongozi imeiagiza Serikali itoe maelezo (Kauli) ya ziada kuhusu suala hilo. Hata hivyo kwa kuwa Waziri husika hakuwepo ukumbini aliagiza Hoja ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji iendelee hadi Waziri atakapokuja.
- Kufuatia uamuzi huo, Wabunge wa Kambi ya Upinzani hawakuridhika na kusimama kuomba miongozo na kupiga makofi wakitaka Waziri wa Elimu atoe Taarifa husika. Kutokana na hali hiyo kuzidi, Naibu Spika aliagiza Mbunge wa Kambi ya Upinzani Mhe. John Mnyika atolewe nje, akifuatiwa na Wabunge wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Aidha, Naibu Spika aliagiza Mhe. Joshua Nassari na Mhe. Ester Bulaya wafikishwe kwenye Kamati ya Maadili kwa kosa la kuanzisha fujo hiyo.

6. Mhe. Mussa Ramadhani Sima	-	CCM
7. Mhe. Njalu Daudi Silanga	-	CCM
8. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga	-	CCM
9. Mhe. Peter Ambrose Lijualikali	-	CHADEMA
10. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara	-	CHADEMA
11. Mhe. Mussa Bakar Mbarouk	-	CUF
12. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka	-	CCM
13. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu	-	CCM
14. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa	-	CHADEMA
15. Mhe. Shally Joseph Raymond	-	CCM
16. Mhe. Zaynab Matitu Vullu	-	CCM
17. Mhe. Hussein Mohammed Bashe	-	CCM
18. Mhe. Janeth Zebedayo Mbene	-	CCM

19. Mhe. Balozi Adadi Rajab	-	CCM
20. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu	-	CCM
21. Mhe. Vedasto Edgar Ngombale	-	CUF
22. Mhe. Said Ahmed Kubenea	-	CHADEMA
23. Mhe. Kasuku Samson Bilago	-	CHADEMA
24. Mhe. Mgumba Omary Tembwete	-	CCM
25. Mhe. Stanslaus Shigh'oma Mabula	-	CCM
26. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma	-	CCM
27. Mhe. Ibrahim Hassanali Raza	-	CCM
28. Mhe. Salim Hassan Turkey	-	CCM
29. Mhe. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka	-	CCM

VIII. KUHITIMISHA HOJA:

Uhitimishaji wa Hoja ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji ulianza kwa Naibu Waziri kujibu baadhi ya Hoja za Wabunge na kufuatia na mtoa hoja, Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambaye alijibu Hoja za Wabunge na kutoa Hoja ya kuliomba Bunge likubali Bajeti ya Wizara yake.

IX. KAMATI YA MATUMIZI:

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi ili kupitisha Vifungu vya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Baada ya kumaliza, Bunge lilirejea, Waziri Mtoa Hoja alitoa Taarifa ya Kazi ya Kamati, Wabunge walihojiwa na kupitisha Bajeti husika.

X. HOJA ZA KAMATI:

Mweyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge alisoma Taarifa ya Kamati yake kuhusu baadhi ya Wabunge kufanya vurugu Bungeni na kudharau Mamlaka ya Spika tarehe 27 Januari, 2016 pamoja na Azimio kuhusu Adhabu kwa Wabunge hao.

Wabunge wafuatao waliunga mkono Hoja husika kwa kuchangia:-

1. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku
2. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete
3. Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangalah
4. Mhe. Goodluck Asaph Mlinga
5. Mhe. Kanali Masoud Ali Khamis
6. Mhe. Sikudhani Yassin Chikambo
7. Mhe. Richard Mganga Ndassa
8. Mhe. Mwanne Ismael Mchemba
9. Mhe. Hafidh Ali Tahir
10. Mhe. Stephen Hilary ngonyani.

Baada ya uchangiaji kukamilika, mtoa Hoja alihitimisha hoja yake na kisha Wabunge walihojiwa kuhusu azimio la Kamati na kulipitisha – adhabu zilizotolewa ni kama ifuatavyo:-

1. Wabunge wasiotakiwa kuhudhuria vikao vya Mkutano wa Tatu na wa Nne wa Bunge ni :-
 - Mhe. Ester Amos Bulaya
 - Mhe. Tundu Antiphas Lissu.
2. Wabunge watakaokosa kuhudhuria vikao vya mkutano wa 3 wa Bunge vilivyosalia ni:-
 - Mhe. Pauline Philipo Gekul
 - Mhe. Godbless Jonathan Lema
 - Mhe. Kabwe Ruyagwa Zitto
 - Mhe. Halima James Mdee.
3. Mbunge atakayekosa vikao 10 vya mkutano wa 3 ni Mhe. John Wegesa Heche.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika alifafanua kuhusu kutokubaliana na maombi ya Wabunge wachache wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kutaka kutoa maoni tofauti kwa kuwa maoni ya Kamati ni yale ya Wabunge walio wengi.

XI. KAULI YA SERIKALI:

Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi alitoa kauli kuhusu wanafunzi wa Diploma maalum ya Ualimu wa Sayansi waliorudishwa Nyumbani kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma.

XII. KUAHIRISHA BUNGE:

Saa 2.20 Usiku Bunge liliahirishwa hadi tarehe 31/5/2016 saa 3.00 asubuhi.

**DODOMA
30 MEI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**